1. Baraza limeboresha mifumo yake ya mapitio ya taarifa za Tathmini na kaguzi za athari kwa mazingira, kwa kuimarisha miundombinu ya TEHAMA kulingana na matakwa ya mfumo wa serikali mtandao (e-Government).

2. Baraza linasimamia miradi inayofanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa njia ya kielektroniki kupitia usajili wa mtandaoni (http://eia.nemc.or.tz). Njia hii inamuwezesha mwekezaji kuanzisha mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) au Ukaguzi wa Mazingira (EA) kupitia mfumo wa usimamizi wa miradi (Project Management System-PMS).

3. Mwekezaji anatakiwa kubainisha mtaalam elekezi aliye na cheti cha utendaji kutoka Baraza kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na ukaguzi wa Mazingira. Orodha ya wataalamu binafsi na makampuni ya wataalamu elekezi inapatikana katika tovuti ya Baraza (www.nemc.or.tz). Kumbuka kuwa wanaoruhusiwa kufanya EIA/EA ni wataalamu elekezi binafsi (Registered EIA/EA Experts) au Makampuni yaliyosajiliwa na Baraza (Registered EIA/EA Consultancy Firms).

4. Kabla ya usajili wa mradi, mwekezaji ahakikishe kuwa mawazo ya wadau yamepatikana kuhusiana na utekelezaji wa mradi kwenye eneo husika. Mawazo hayo yahusishe sekta husika na viongozi wa Halmashauri, Kata, Mitaa, Kijiji na Kitongoji. Hii pia ihusishe mawazo ya wananchi kwenye maeneo yanayozunguka eneo la mradi. Uwasilishaji wa taarifa za awali kwa Baraza (Scoping Report) uambatane na uwasilishaji wa taarifa zinazothibitisha ya kuwa wadau wamepokea taarifa hiyo ya awali (evidence of service).

5. Mwekezaji kwa kutumia mtaalamu elekezi wa mazingira, atatakiwa kuzingatia mambo muhimu ili kuhakikisha utekelezaji endelevu wa miradi inaayokusudiwa ikiwa ni pamoja na maswala ya umiliki wa ardhi, uwiano wa mradi na mpango wa ardhi kwenye eneo husika. Pia eneo lililoainishwa lisiwe na migogoro au ahakikishe migogoro iliyokuwepo imepatiwa ufumbuzi.

6. Zifuatazo ni hatua zinazopaswa kufuatwa wakati wa usajili wa miradi kwa njia ya mtandao (on line registration).

i. **Hatua ya kwanza ni: Usajili (Registration):** Mwekezaji hujaza fomu ya usajili kwa njia ya mtandao na kulipa ada ya usajili kwa muhtasari wa mradi.

ii. **Hatua ya pili ni: Uchunguzi wa kina (Scoping):** Mwekezaji kwa kushirikiana na Mtaalamu elekezi atawasilisha Mawanda ya mradi (Scoping report) pamoja na Hadidu za Rejea (ToR) zitakazoonyesha jinsi tathmini hiyo itakavyofanyika. Baraza litapitia hadidu za rejea na taarifa za mawanda ya mradi na kuzithibitisha, kuzikataa au kuelekeza kufanyiwa maboresho.

iii. **Hatua ya tatu ni: Tathmini ya Athari kwa mazingira:** Mwekezaji atalipia gharama ya kupitia mradi na kuingiza ripoti ya TAM/Ukaguzi wa mazingira kupitia mfumo wa PMS.

iv. **Hatua ya nne ni: Mapitio ya taarifa za mradi (Review):** Baraza litatembelea eneo la mradi husika, kuwasiliana na wadau wa mradi na kupata maoni yao. Hii hufuatiwa na kikao cha Kamati ya Ushauri (Technical Advisory Committee meeting).

v. **Hatua ya tano ni: Mapendekezo ya Kamati ya ushauri (Recommendations of the Technical advisory Committee TAC):** Mshauri elekezi atawasilisha andiko lililoboreshwa kwa Baraza likijumuisha maboresho yaliyopendekezwa na wadau na kamati na kisha kuingizwa kwenye mfumo.

vi. **Hatua ya sita ni: Kuwasilisha mapendekezo kwa Mhe. Waziri mwenye dhamana ya mazingira (Submission of recommendations to the Minister responsible for Environment):** Baraza litawasilisha mapendekezo ya mradi kwa Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kwa hatua zaidi.

vii. **Hatua ya saba ni: Kuidhinishwa kwa taarifa ya TAM/Ukaguzi wa mazingira (Approval of the EIS/EA):** Baada ya kusainiwa kwa Cheti na Waziri, kitarejeshwa NEMC kwa ajili ya kukabidhiwa mwekezaji. Hata hivyo, Waziri anaweza kuidhinisha au kutoidhinisha TAM/Ukaguzi wa Mazingira ndani ya siku 30 kulingana na Sehemu ya 92(1) ya EMA Sura 191.

viii. **Hatua ya nane ni: Kuidhinishwa kwa mradi na kutoa Cheti (Issuance of Certificate):** Waziri mwenye dhamana ya mazingira ataidhinisha uendelezaji wa mradi kwa kusaini cheti kwaajili ya kukabidhiwa kwa mwekezaji. Cheti huambatana na masharti ya jumla na mahsusi ya kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa mradi.

7. Baraza kwa nyakati tofauti litafanya ukaguzi wa eneo la mradi ili kuhakikisha ya kuwa mradi unatekelezwa kwa kuzigatia masharti yaliyotolewa kwenye cheti ikiwa ni pamoja na matakwa ya Sheria ya Mazingira na kanuni zake.

8. Wawekezaji wako huru kuchagua ofisi ya NEMC ambayo mradi utasajiliwa na kufanyiwa mchakato ikiwa ni pamoja na Makao Makuu au Ofisi za Kanda kwa kupitia mfumo wa usajili wa miradi kieletroniki. Mwekezaji anaweza kupata ufafanuzi wa masuala yanayohusu usimamizi wa Mazingira kupitia ofisi za NEMC zilizoainishwa hapa chini. Lengo la kuwa na Ofisi za Kanda ni kusogeza huduma karibu na wananchi na pia kuhakikisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira katika mikoa unasimamiwa kikamilifu. Hivyo Kanda zina uwezo wa kusajili miradi na kusimamia masuala mengine ya mazingira yatakayo jitokeza katika mikoa husika kwa ujumla wake.

## BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA LINA MAKAO YAKE MAKUU JIJINI DODOMA NA OFISI 13 ZA KANDA

| Na. | MAKAO MAKUU | ANUANI |
|---|---|---|
| | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) | Mkurugenzi Mkuu,<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC)<br>Kambarage Tower, Ghorofa ya 6<br>P.O.Box 2724, Dodoma Tanzania<br>Simu: +255 26 2960098, +255 713 608 930<br>Nukushi: +255 22 2774901<br>WhatsApp: +255 737 796 252<br>Tovuti: www.nemc.or.tz<br>Barua pepe: dg@nemc.or.tz |
| | **OFISI ZA KANDA** | |
| 1 | Kanda ya Ziwa inayohusisha Mikoa ya Mwanza ,Simiyu, Mara, Shinyanga na Geita.<br>Ofisi zake ziko | PSSSF Front Wing, 6th Floor, Plot No. 17/1, 17/2 and 18, Barabara ya Kenyata,<br>P.O. Box 11045, Mwanza<br>Phone. 0782296112, 0713296112 |
| 2 | Kanda ya Kaskazini inayohusisha Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.<br>Ofisi zake ziko Mkoa wa Arusha Mkoa wa Mwanza. | Makutano ya Makongoro-Goliondoi, Mzunguko wa Ngorongoro, Kitalu Na. 055019/1 and 055019/6, Jengo la utalii la Ngorongoro, Ghorofa 6<br>S.L.P 1041 Arusha<br>Simu: +255738064966, 0784333583, 0655333538<br>Barua pepe:<br>nemcarusha@nemc.or.tz |
| 3 | Kanda ya Nyanda za juu Kusini inayohusisha Mikoa ya (Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe).<br>Ofisi zake ziko Mkoa wa Mbeya | Karume Avenue,<br>S.L.P 6215, Mbeya,<br>Telephone 0713390379<br>Barua pepe:<br>nemcmbeya@nemc.or.tz |
| 4 | Kanda ya Kati inayohusisha Mikoa ya Dodoma, Tabora na Singida. Ofisi zake ziko Mkoa wa Dodoma | Jengo la PSPF Dodoma Plaza, Ghorofa ya 6<br>S.L.P 2724, Dodoma.<br>Simu. +255262963859/860<br>Barua pepe:<br>nemcdodoma@nemc.or.tz |
| 5 | Kanda ya Kusini Mtwa inayohusisha Mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Lindi . | Raha leo Complex (Jengo la NHC, Ghorofa 3)<br>S.L.P 1259, Mtwara.<br>Simu. +255232334683, 0767153776, 0621989301<br>Barua pepe.<br>nemcmtwara@nemc.or.tz |
| 6 | Kanda ya Magharibi inayohusisha Mikoa ya (Kigoma, Katavi, Tabora na Kagera )<br>Ofisi zake zipo Kigoma | Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya 1, Kitalu Na. 100 Nyumba na 1, Mtaa wa Mnarani.<br>P.O. Box 974, Kigoma Ujiji.<br>Simu.0713566367<br>Barua pepe:<br>nemckigoma@nemc.or.tz |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Kanda ya Mashariki Kusini inayohusisha Mkoa wa Dar es salaam, wilaya ya Mkuranga, Kigamboni, Mafia, Kisarawe na Kibiti | Mtaa wa Regent. Kitalu No. 28-30, S.L.P 63154<br>Simu. +25522 277 4889, 0756664775<br>Dar es salaam Tanzania |
| 8 | Kanda ya Mashariki Kaskazini inayohusisha Wilaya ya (Kinondoni, Ubungo and Kibaha). Ofizi zake ziko Mkoa wa Dar es salaam | Regent St. Kitalu No. 28-30, S.L.P 63154<br>Simu. +25522 277 4889, 0742 774735<br>Dar es salaam Tanzania |
| 9 | Kanda ya Morogoro Rufiji | S.L.P 1342, Morogoro<br>Simu: 0784 506267/ 0738 953787<br>Barua Pepe: nemcmorogoro@nemc.or.tz |
| 10 | Kanda ya Ilala | Regent St. Plot No. 28-30, S. L. P 63154<br>Simu. +25522 277 4889, 07846303539.<br>Dar es salaam Tanzania |
| 11 | Kanda ya Temeke | Regent St. Kitalu No. 28-30, S.L.P 63154<br>Simu. +25522 277 4889,0676 164088<br>Dar es salaam Tanzania |
| 12 | Kanda ya BAGAMOYO inayohusisha Mkoa wa Tanga pamoja na Wilaya ya Bagamoyo | Regent St. Plot No. 28-30, S.L.P 63154<br>Simu.+25522 277 4889, 0753402334<br>Dar es salaam Tanzania |
| 13 | Kanda ya ziwa Victoria Magharibi. | Ofisi zake zipo Geita<br>Simu: 0685 117589 |

## MWEKEZAJI ANAPASWA KUZINGATIA MASUALA YA FUATAYO WAKATI WA USAJILI WA MIRADI

1. Mwekezaji anatakiwa kuchagua mtaalamu mwelekezi wa Mazingira aliyesajiliwa na NEMC kwenye orodha ya watalaam elekezi inayopatikana kupitia tovuti ya Baraza www.nemc.or.tz.
2. Kazi atakayo kabidhiwa na mtaalamu mwelekezi iwiaane na Cheti cha usajili wake (Certificate of Practice).
3. Mwekezaji kutoa taarifa sahihi juu ya mradi kwa mtaalamu mwelekezi ili aweze kukushauri ipasavyo, pia kukikisha taarifa anazoziwakilisha NEMC ni sahihi na kamilifu.
4. Mwekezaji kuhakikisha mshauri mwelekezi ameweka namba yako ya simu/mawasiliano yako katika taarifa za mradi wako anazoziwasilisha NEMC.
5. Mawasiliano yote kati ya mwekezaji na NEMC yatafanywa na mwekezaji na nakala kwa mtaalam mwelekezi. Endapo mwekezaji utapendelea mtaalamu mwelekezi akuwakilishe, basi ni lazima Mtaalam apatiwe barua ya kuruhusu kukuwakilisha NEMC.


**Mkurugenzi Mkuu**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**
Kambarage Tower, 6th Floor
P.O Box 2724, Dodoma,Tanzania,
Tel: +255 26 2960 098, +255 713 608 930,
Nukushi: +255 22 277 4901, Whatsap: +255 737 796 252
Email: dg@nemc.or.tz | Website: www.nemc.or.tz

@nemctanzania
www.nemc.or.tz
Namba ya dharura: 0800110116
NEMCTVTanzania


#MazingiraYetuUhaiWetu

## Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)



# HATUA ZA KUZINGATIA WAKATI WA KUFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KWA MRADI KUTHIBITISHWA NA KUPATA CHETI